TOSCI

TANZANIA OFFICIAL SEED CERTIFICATION INSTITUTE

**Tarehe 31 Julai, 2025**

## TANGAZO KWA UMMA

## BEI YA MBEGU ZA MAHINDI ZILIZOTHIBITISHWA UBORA KWA MPANGO WA RUZUKU YA SERIKALI MSIMU WA 2025/2026

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kutekeleza mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbegu bora za mahindi kwa msimu wa 2025/2026. Katika kufanikisha mpango huo, Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji ikiwa ni pamoja na kutoa bei elekezi, kusajili makampuni ya mbegu na mawakala wa usambazaji wa mbegu pamoja na wakulima wanufaika wa mpango huo.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbegu za Mahindi Zilizothibitishwa Ubora kwa Msimu wa Kilimo wa Mwaka 2025/2026, bei elekezi kwa aina mbalimbali za mbegu za mahindi kuanzia tarehe 01 Agosti, 2025 ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 1:** Bei elekezi ya mbegu bora za mahindi kwa msimu wa 2025/2026

| **Aina ya Mbegu** | **Bei ya Ukomo (TZS/2kg)** | **Bei ya mkulima yenye ruzuku ya Serikali (TZS/2kg)** | | **Ruzuku ya Serikali (TZS/2kg)** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Bei ya chini** | **Bei ya juu** | |
| Mbegu ya uchavushaji huria (OPV) | 9,500 | 7,000 | 7,700 | 2,500 |
| Mbegu chotara (hybrid) ya muda mfupi na wa kati | 17,000 | 14,000 | 14,700 | 3,000 |
| Mbegu chotara (hybrid) ya muda mrefu | 18,000 | 14,500 | 15,200 | 3,500 |

Orodha ya aina ya mbegu za mahindi zilizosajiliwa na TOSCI zitakazouzwa kwa mpango wa ruzuku zimeainishwa kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** Orodha ya aina za mbegu za mahindi zitakazouzwa kwa mpango wa ruzuku msimu wa 2025/2026

a) Aina ya mbegu zinazochavushwa huria (open pollinated varieties OPVs)

| Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NATA K 6Q | 6 | TMV-2 | 11 | T105 |
| 2 | NATA K 8 | 7 | SITUKA M1 | 12 | T104 |
| 3 | TZM 523 | 8 | Kilima | 13 | SITUKA M2 |
| 4 | LISHE K1 | 9 | Staha | | |
| 5 | Bora | 10 | TMV - 1 | | |

b) Aina ya mbegu chotara (hybrid varieties) zinazokomaa kwa muda mfupi na wa kati

| Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | NATA H 105 | 41 | MERU VAH 519 | 68 | ZMS 528 |
| 15 | UH 6303 | 42 | MERU HB 405 | 69 | EAS 5019 |
| 16 | UH 615 | 43 | MERU HB 513 | 70 | ADV 2308W |
| 17 | DK 8031 | 44 | MERU HB 623 | 71 | MERU HB 515 |
| 18 | DKC 80-33 | 45 | WE 4114 | 72 | KS H 519 |
| 19 | DKC 80-53 | 46 | SC 303 | 73 | H 6213 |
| 20 | SY 6444 | 47 | SC 403 | 74 | H 624 |
| 21 | SY 5054 | 48 | SC 419 | 75 | PAN 4M- 11 |
| 22 | PAN-3M-05 | 49 | SC 513 | 76 | P 2848 W |
| 23 | 30G19 | 50 | SC 555 | 77 | ZR 8643 |
| 24 | P 3812 W | 51 | TZH 536 | 78 | UHS 401 |
| 25 | PAN 15 | 52 | TZH 538 | 79 | UH 6305 |
| 26 | PAN 3M-05 | 53 | KH 500-43A | 80 | UHS 5350 |
| 27 | PAN 53 | 54 | EAS401 | 81 | LAKE 401 |
| 28 | PAN 4M-19 | 55 | WH 509 | 82 | LAKE 601 |
| 29 | PHB 3253 | 56 | WH 605 | 83 | GV 673A |
| 30 | ETG M 601 | 57 | WH 403 | 84 | MG1063 |
| 31 | Kaspidi | 58 | WH 505 | 85 | MG 1055 |
| 32 | Lubango | 59 | ZMS 606 | 86 | P3531W |
| 33 | H 513 | 60 | ZMS 405 | 87 | MERUHT1 |
| 34 | DH 04 | 61 | ZMS 402 | | |
| 35 | H 625 | 62 | ZMS 520 | | |
| 36 | H 628 | 63 | AMH500 | | |
| 37 | H 614 | 64 | WE4102 | | |
| 38 | MAMSH 457 | 65 | SC 657 | | |
| 39 | MAMSH 458 | 66 | TZM 523 | | |
| 40 | MERU VAH 517 | 67 | ZMS 520 | | |

c) Aina ya mbegu chotara (hybrid varieties) zinazokomaa kwa muda mrefu

| Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu | Na. | Aina ya Mbegu |
|---|---|---|---|---|---|
| 88 | DK 777 | 93 | ETG M 601 | 98 | DKC 97 - 09 |
| 89 | DKC 90-89 | 94 | ZMS 720 | 99 | ZMS 623 |
| 90 | PAN 691 | 95 | H 6302 | 100 | ZMS 721 |
| 91 | SC 719 | 96 | DKC 88 - 45 | | |
| 92 | ZMS 638 | 97 | PAN 9M - 91 | | |

Wafanyabiashara wa mbegu ikiwemo makampuni ya uzalishaji, uagizaji na mawakala wa kuuza mbegu wanatakiwa kuzingatia bei elekezi kwa kila kituo cha mauzo kilichosajiliwa na TOSCI pamoja na taratibu nyingine zilizoainishwa kwenye Mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mahindi kwa msimu wa kilimo wa 2025/2026. Aidha, wakulima wote ambao hawajasajiliwa kwenye mfumo wa kidijiti wa usajili wa wakulima wanapaswa kusajiliwa kwenye ofisi za kilimo ngazi ya Kijiji, Kata, Halmashauri au kwenye vituo vya mauzo ya mbegu bora za mahindi kupitia mawakala waliosajiliwa ili waweze kunufaika na mpango wa ruzuku ya mbegu bora za mahindi.

Imetolewa na:

Nyasebwa E. Chimagu
**MKURUGENZI MKUU**